# TUJIFUNZE MAANDIKO KWA MIFANO.

**Na S. Z. Mwanshanullah**

**SOMO KUHUSU KANISA.**

**1) Tunatazama kila mahali na kuona watu mbali mbali na kila mahali watu waabudu, na wote wanategemea kufika mbinguni, je, ni kweli?**

Wengine wanasema mimi ni wa ------- na wengine ni wa ------na wengine ni wa -----.

Je, Mungu anafurahia madhehebu?

Watu wengi wanasema, jina la kanisa si kitu bora imani yako na matendo, jina la kanisa ni jina tu, ewe ndugu yangu sikiliza mfano huu:

Wewe ni mume wa ----au mke wa --------

Kwa mfano wewe nyumbani mwako una watoto wawili, wakwanza ni Sala Sanga na wapili ni Joseph Sanga. Na mke wako ana mimba ya mtoto watatu, sasa wewe mwanaume unaamua kuondoka pale nyumbani kwenda kutafuta mahitaji, na unaporudi nyumbani kumbe mwenzio ameisha jifungua mtoto wa kiume anaitwa Maiko Shelite, na wewe bwana unaitwa Saidi Sanga, na huyu mtoto wako anaitwa Maiko Shelite.

Je, utafurahi jina la ukoo la mtu mwingine? Unapomuuliza mke wako anasema nilipenda tu kumpa jina la ukoo wa jirani yetu, lakini mtoto ni wako hilo ni jina tu. Je, utafurahi? Au je, utamwelewaje huyo mwanamke? Mungu amemleta mwokozi ambaye jina lake Kristo, Yoh. 3:16, na watu hawataki kuliiita kanisa jina hilo, ila kwa majina ya miji na majina ya watu na majina mengine, 1 Kor. 1:10-13.

Ndugu yangu wokovu haupatikani nje ya kanisa lake Mdo. 4:12. Mke wako akimpa mtoto wako jina la ukoo wa mtu mwingine utamwita mzinzi, je wewe ulie jipa jina lingine la kanisa Mungu akuiteje?

Neno “kanisa” maana yake ni walioiitwa (H.S.) waliookoka au watakatifu, au waumini.

**2) Sasa basi hebu angalia mfano huu.**

Kanisa la Kristo

Watakatifu wa Kristo

Kanisa la Momonizimu

Watakatifu wa Momonizimu

Kanisa la Lokrati

**3) Somo Kuhusu Ubatizo**

Watu wengine wanafikiri kuwa ubatizo wo wote ule ni halali bora una majina matatu, wengine wanasema kitabu cha Matendo 16:30-34 hapo kuna mlinzi wa gereza aliyebatizwa yeye na nyumba yake usiku ule ule, inamaana alinyunyizwa yeye pamoja na nyumba yake.

Sasa tuone neno hili “ubatizo” maana yake nini, neno hili ubatizo maana yake ni zamisha. Kwa kiyunani yaani kama analoweka kamba husema “baptizo” yaani amezamisha, na kwa sababu neno ubatizo lilikuwa lina eleweka toka mwanzo, kama tunavyoelewa sisi kuhusu kuzama, hivyo ilikuwa si lazima waseme walikwenda mtoni.

**4) Sikiliza Mfano Huu.**

Kuna watu 35 na mkubwa wao waende vitani, walipofika kule walianza kupigana wakapigwa wao 15 wakafa, wakachukua maiti yao wakachimba kaburi, wakazika. Tena wakafa 14 wakachimba kaburi wakazika, tena wakafa 4 nao wakazikwa, je, hawa 4 walizikwa vipi? Mbona hawakuchimba kaburi? Tena mzee akikutuma ukaloweke kamba mtoni, halafu wewe uende kunyunyizia je, utakuwa umeloweka? Au mama akikutuma uloweke mahindi halafu wewe unachukua mahindi na kuyatandaza penye mjamvi na kuyanyunyizia, je, mama atakapokuja atasema umeloweka?

Neno **ubatizo** lilitamkwa kwa lugha ya kiyunani, **baptize. Neno nyunyiza ni rantizo; na neno mwagia ni cheo.**

Sasa chagua wewe mwenyewe Yesu alitumia lipi hapo.

**Rantizo, baptizo, cheo**.

**5) Mfano mwingine “Ubatizo”**

Biblia inasemaje? Yoh. 3:1-6 ubatizo umefananishwa na kuzaliwa kwa mama, kwa hiyo kama kwa mama ulizaliwa kichwa tu, basi peleka kichwa chako wakanyunyizie.

Tena umetajwa kuzika, kwa hiyo tunajua kuwazika ni lazima uchimbe shimo na kuweka maiti ndani halafu kufukia je, kwa nini usizike kichwa na mwili ukabakia nje? Kol. 2:12, na kama mbatizaji amechukua maji kwenye kikombe, je, kunauwezekano kutelemka wote wawili ndani ya kikombe? Mdo. 8:34-38; Mt. 3:13-16.

**6) Kuokoka**

Watu wengi wanapinga neno hilo kuwa kuokoka mpaka siku ya mwisho. Sikiliza mfano huu:

Mtu mmoja alisafiri kutoka Kushi kwenda Samaria, kabla ya kufika Samaria akiwa njiani alitokewa na nyuki, akakimbia na bahati mbaya akaangukia ndani ya shimo, humo ndani mlikuwa na simba, akawa anaisikia sauti ya yule mtu, akaanza kumfuata na yule mtu alipogeuka nyuma alimuona simba na alipotazama juu alimuona mtu, huyo mtu alimrushia kamba nae akadaka ile kamba akavutwa mpaka nje na yule simba akawa amefika mahali alipoangukia yule mtu. Je, yule mtu alipotoka kwenye lile shimo na kuwa huru mbali na simba, je, atasemaje? Bila shaka atasema ameokoka kutoka katika hali ya hataari.

Kuokoka ni kuacha dhambi, Mdo. 16:30-34.
Kuokoka lazima uwe ndani ya kanisa lake, Kol. 1:13; Kol. 1:18.

**7) Kuimba Kwa Kutumia Vyombo (Vya Muziki H.S).**

Yesu aliimba, lakini hatuoni sehemu yo yote ile kuwa Yesu alichukua ngoma au filimbi, gitaa, kinubi, zeze, matari, au kucheza. Katika Agano la Kale kuna mtu aliamua yeye akiwa ni mfalme kuwa waimbe nyumbani mwa Bwana kwa kutumia vyombo, 1 Nya. 23:4-5; 1 Nya. 25:6; Zab. 33:1-4; Zab. 150:1-6. Hapo tunaona kuwa ni amri ya mfalme wala sio amri ya Mungu. Tena Mungu baada ya kuona wana wa Israeli wanaendelea na vitu vile, alikataa kwa kutumia kinywa cha Amosi, Amo. 5:23; 6:5. Katika Agano la Pili (yaani Agano Jipya) hatuoni mahali po pote pale panapo sema tuimbe kwa kutumia vyombo. Inatakiwa tutumie pumzi zetu, Kol. 3:16; Efe. 5:19, Mt. 26:30.

Kuna mzee mmoja alikuwa na watoto wawili mmoja wa kiume na mwingine wa kike, wote hawa waliishi mbali na baba yao, siku moja waliondoka kwenda kumsalimu baba yao, walipofika kule walimkuta baba na mama wakiwa ni wazima, wakapokea kazi ya kuvuna mahindi, wakavuna siku 1 siku 2 na ya 3 wakamaliza kazi hiyo; sasa baba na mama wakaona ni afadhari wawape zawadi, wakawaita wale watoto wao wakawapa sh. 6,000/-. Wale watoto wakashukuru na kusema ahsante wakawa na furaha kubwa mionyoni mwao na kwa sababu wanafuraha, na ile zawadi. Je, ni vizuri wachukue ngoma au filimbi na kuanza kumpigia baba na mama na kucheza? Watu wengi wanasema siyo heshima. Ni kweli siyo heshima! Sasa ikiwa baba tunamwogopa hata kumpigia vyombo vya miziki. Je, Mungu si zaidi? Bila shaka watu wengi wanafuata viongozi wao, bila kufuata, maandiko Mt. 22:29; 15:7-9; Tit. 1:16. Ndugu yangu kumchezea Mungu acha!